© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Himdi zote ni zenye kumthubutikia Mola pamoja na kumtaka Yeye msamaha na maghfira na twajilinda Kwake Yeye na shari za nafsi zetu na vitendo vyetu viovu, alo ongozwa ni Allaah hakuna wa kumpoteza na alopotezwa na Yeye hakuna wa kumuongoza na twashuhudia kuwa hapana wa kuabudiwa isipokuwa Yeye hana mshirika na Mtume Muhammad (Sallallaahu 'alayhi wasallam) ni mjumbe wake; waba'du:

Huu ni mukhtasari wa makala kuhusu Manhaj yetu, Manhaj ya as-salaf, yaloandikwa na mmoja katika wanazuoni wetu wa ki-salafi, sheikh saleem bin Eid al-Hilaalee (Hafidhahullaah) katika kubainisha maana ya neno "salaf", na nikina nani hao na Manhaj gani ambayo wanayo jinasibisha nayo.

Kwanza kabisa - tamko hili la "salaf" katika lugha ya kiarabu na katika istilahi ya wanazuoni hutumiwa kwa zama zipi? Ni wajibu kwa mwenye kufuata Manhaj ya salafi awe katika uangalifu juu ya huja zilizo wazi. Na hili ndilo sharti lake Mola (Subhaanahu wa ta'aalah). Aliposema kama ilivyofasiriwa:

قُلْ هَٰذِهِۦ سَبِيلِىٓ أَدْعُوٓا۟ إِلَى ٱللَّهِ ۚ عَلَىٰ بَصِيرَةٍ أَنَا۠ وَمَنِ ٱتَّبَعَنِى ۖ

Sema (Ewe Muhammad, kuwaambia jamaa zako) Hii ndiyo ndia yangu ninayoilingania katika ndia ya Allaah kwa ujuzi wa kweli; mimi na kila ambaye ni mwenye kuifuata ndia kama hii. [Soorat Yusuf 12:108]

Huu ndiwo ulinganizi wake. Na kilma hichi cha salaf katika lugha ya kiarabu, maana yake ni watu ambao walopita wakatangulia kwa ilmu, kwa kuamini,

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

kwa ubora na kwa wema. Akasema mwanachuoni wa lugha, ibnul Mandhur katika kamusi yake ya lugha - "lisaanul arab", tamko la salafi lamaanisha watu walotangulia katika baba zako na jamaa zako wa karibu ambao walokupita ki-umri na ubora. Na ndio ukaona lile pote la kwanza katika taabi'een wakaitwa watu wema walotanguliya, As-Salaf as-Saalih. Na vile vile neno lake Mtume (Sallallaahu 'alayhi wasallam) katika kufafanua tamko hili la As-Salaf alipomwambia mtoto wake faatimah:

"Mtu mwema uliyoje utakae nitangulia baada yangu mimi" [Muslim no. 2450]

Ama tamko hili katika istilahi ya wanazuoni, ni sifa ambayo ilokhusishwa kwa Maswahaba na vilevile wanaingia wengineo wasokuwa wao walofuata nyenendo za Maswahaba. Akasema mwana chuoni al-Qalshaaniyyu, "as-salafu as-saalih ni lile pote la kwanza lilotopea katika ilmu ya wenye kufuata uongofu wa Mtume (Sallallaahu 'alayhi wasallam) na wenye kuhifadhi sunna zake, ambao Mola aliwachagua kufuatana na Mtume Wake na akawachagua kuisimamisha dini yake wakawarithi wao viongozi wa ummah, Ma'Ulamaa wakapigana jihadi katika ndia ya Allaah kwa mali zao na nafsi zao, kama walivyosifiwa na Allaah katika Qur'aan katika Suratil fat-h aya ya 29, na Surat an-Nisaa' aya ya 115 na Mola katika aya hii akatangaza adhabu kali kwa atakae wakhalifu na akafuata ndia nyengine isiyokuwa yao. Kwahiyo ni wajibu wetu kuwafuata na kuwatakia msamaha na wakakubaliana watu wa 'ilmu wa mwanzo na wasasa kuhusu maana ya tamko hili la As-Salaf kama tulivyolieleza, na hakika wameliambatisha watu wa 'ilmu tamko hili katika istilahi na karne tatu bora ambazo Mtume (Sallallaahu 'alayhi wasallam) alizisifu. Huo ulikuwa ni wakati wa Maswahaba na walokuja baada yao ndilo kusudio la tamko la As-Salafi.

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Amesema Imaam al-Ghazaalee katika kulieleza tamko la salafi: "Makusudio ya Salaf ni madh-hab ya Maswahaba na Taabi'een. Na Ameerul-Mu'mineen wa hadeeth, al-imaam ibnu-Hajar amesema katika kulifasiri tamko la as-Salaf: "Makusudio yake ni maswahaba na wale walokuja baada yao wakafuata mwendo wa maswahaba." [Fat-hul Baari vol 6 Uk.66]

Amepokea Imaam Muslim kutoka kwa Muhammad bin 'Abdillah kuwa amesema: "Nilimsikia 'Ali bin Shaqeeq akisema, 'Nilimsikia 'Abdullaah bin al-Mubaarak akisema mbele za watu, 'Wacheni musichukue hadeeth ya 'Amru bin Thaabit, kwani yeye alikuwa akitukana ma-Salaf', na muradi wake hapa ni maswahaba." Akasema al-imaam al–Auza'ee: "Isubirishe nafsi yako katika kufuata Sunnah na usimame pale walipo simama watu na useme yale waliyoyasema watu na ujizuie na yale waliyojizuia nayo watu na ufuate ndia ya watu wako wema walotangulia kwani itakutosheleza". Na muradi wa watu wema hapa, ni Maswahaba (Allaah awaelee radhi). Kwahiyo yatosheleza kulingana na aqwaal zilizo pita yakuwa tamko la salafi kusudio lake ni zama za Maswahaba na walokuja baada yao wakafuata mwendo wao. Ama tamko hili katika kutumika kwake katika upande wa zama au muda ni tamko ambalo hukusudiwa kwa zile qarne tatu bora ambazo Mtume (Sallallaahu 'alayhi wasallam) alosema: "Bora ya watu ni wa qarne au zama zangu, kisha ni wale watakao kuja baada yao, kisha watakao kuja baada yao".

Na wala haimaanishi yakuwa madh-hab ya Salafi yameshapita kwa sababu ya kupita karne zile tatu, Laa! bali kila mwenye kufuata mwendo wao kwa wema pia yumo katika twariqa ya ki-Salafi kama tunavyoona katika tareekh yakwaba mwisho wa zama hizo hizo za maswahaba kulitokea vipote viovu pamoja na kuwa walikuwa katika karne bora. Kwa hivyo linadhihiri tamko hili hapa kuwa kila anae fuata mwenendo walokuwa nao maswahaba kwa wema mpaka siku ya kiyama, na wale waloshikamana na 'aqeedah swaheeh na mwenendo alokuwa nao Mtume na maswahaba zake pasi na kukhitalifiana.

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Kwa hivyo Manhaj ya Salafi ni sifa Nzuri ya Muislamu kujipamba nayo wala si jambo geni lililozuliwa kama wanavyo dai baadhi ya watu. Amesema al Imaam ibnu Taymiyyah:

"Wala si aibu kwa yule mwenye kudhihirisha madh-hab ya Salafi na kujinasibisha nayo na kujifakhiri nayo, kwani hayakuwa madhhab ya Salafi isipokuwa ni madh-hab ya haki". [Majmoo'-al Fataawa vol 4 Uk.149]

Madh-hab ya as-Salafi na mustaqbal wa kiislam

Hakika zimethubutu aysa nyingi na hadeeth mutawaatir zenye kueleza na kutowa bishara kwa mustaqbal wa Uislamu na kurudi kwa 'Izza yake kama zamani. Na nikina nani ambao watakao kuirudisha 'Izza hiyo. Hakika zimetudhubutukia yakuwa wale ambao watakao regesha 'Izza hii ni wale ambao watakaokuwa katika Manhaj hii ya as-Salafi kama ilivyokuja katika hadeeth ya Mtume (Sallallaahu 'alayhi wasallam). Amepokea swahaba Hudhaifah ibn-ul Yamaani (Radhiallaahu 'anhu) aliesema yakwamba amesema Mtume (Sallallaahu 'alayhi wasallam):

"Utakuja kwenu nyinyi Utume kwa kadri Mola Atakavyo taka, kisha Auondoe pindi atakapo kuondoa, kisha alete utawala kwa misingi ya Manhaj ya Mtume, ukae kiasi cha Mola Atakavyo taka, kisha auondoe pindi atakapotaka kuondoa, kisha uje utawala wa kimabavu, kisha auondoe, kisha alete utawala wa nguvu auondoe kisha arudishe utawala ambao utakwenda kwa manhaj ya Mtume (Sallallaahu 'alayhi wasallam), kisha akanyamaza."

Kwa hiyo yaonyesha kuwa 'Izza ya Uislamu itarudi kwa kurudi ile khilafah ambayo itakuwa katika mfumo wa Mtume (Sallallaahu 'alayhi wasallam), na nikina nani watakao kuirudisha khilfah ya kiislamu tena? Si Salaf as-Saalih waloshikamana na nyenendo za maswahaba? Kwa hakika yabainika waziwazi

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

yakuwa hawa ndiwo watakao irudisha khilafah ya kiislamu na ndiwo ambao walo shikamana na Manhaj ya as-Salafi.

Ndia ya Manhaj ya as-Salafi katika kuubadilisha Ummah:

1. At-Tasfiyah (ama kusafisha)

Hakika mambo haya hayawezi kupatikana isipokuwa kwa kuregea Waislamu katika dini yao halisi iliyotakasika na kila aina ya itikadi na vitendo vichavu kwa neno lake Mtume Muhammad (Sallallaahu ʻalayhi wasallam). Katika hadeeth yake:

> ***"Mutakapo fanya biashara ya iina na mukajishughulisha na mifugo na makulima na mukaata jihaad, Allaah (Subhaanahu wata'aalah) Atawasallit nyinyi kwa kuwatia dhulli na unyonge mpaka murudi katika dini yenu."*** [Fat-hul baari 6.610].

Na twakusudia kwa tamko hili la at-Tasfiyah yaani kusafisha mambo yafuatayo:

a. kuisafisha ʻaqeedah ya kiislamu na kila fikra mbovu zilizotoka katika vipote vya upotofu kama Mu'tazilah, Jahmiyyah, Khawaarij, Murji'ah, Soofiyyah, Shi'ah na kadhaalika (n.k). Kwa mfano kuzikanusha Sifa za Allaah Alizojisifu nazo katika Qur'aan, au kuzipotoa, au kutokubali kutumia hadeeth Aahad katika masala yanayofungamana na ʻaqeedah na baadhi ya nyuradi za ki-Soofee zilizojaa shirk.
b. Kutakasa madh-hab ya kiislamu na jihaad za kimakosa zenye kukhalifu Qur'aan na Sunnah za Mtume wake (Sallallaahu ʻalayhi wasallam).

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

c. Kuvitakasa vitabu vya tafsiri ya Qur'aan na hadeeth za Mtume (Sallallaahu 'alayhi wasallam) Kutokamana na riwaya dha'eef na maudhoo' na Israailiyyaat.
d. Kutakasa vitabu vya ki-lugha kutokamana na uharibifu ulofanywa na baadhi ya wanazuoni wakaribu waloathirika na fikra za ki-Mu'tazilah na kudai kuwa lugha ya kiarabu imegawanyika mara mbili: **[Haqeeqah na Majaaz]**
e. Kuitakasa tareekh ya kiislamu kutokamana na tuhma na urongo mwingi ulotiwa ndani yake na maadui wa kiislaumu kama mustashriqiin (Orientalists). Na dalili ya kisheria yenye kueleza umhimu wa Tasfiyyah ni hadeeth yake Mtume (Sallallaahu 'alayhi wasallam) aliposema:

"Wataibeba ilmu hii (yaani dini) watu wema waadilifu watakao kataa uharibifu wa wale watakao taka kuharibu (dini hii) na kuleta urongo ndani yake."

Ushahidi waonyesha yakuwa ahlul ilmi ndiwo watakaoshika bendera ya Tasfiyyah na kuutakasa Uislamu na kila uchafu ulotiwa ndani yake ili urudi kama mwanzo ulipoteremshwa kwa Mtume Muhammad (Sallallaahu 'alayhi wasallam) kwa uadilifu.

2. Jambo la pili ni At-Tarbiyyah:

Kwa hakika at-Tasfiyyah haiwezi kuleta matunda yake pasi na at-Tarbiyyah (Malezi) ya kuwalea Waislamu katika malezi ya kiislamu swafi na 'aqeedah mbovu na kusudio la tarbiya hapa nikufikishwa nafsi ya mwanadamu katika ukamilfu uloandaliwa polepole .Na Mlezi wa kihakika ni Allaah (Subhaanahu wata'aalah) kwa sababu Yeye ndiye Muumbaji na ndiye Ampaye mwana-

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

damu na Akamtengeneza ki-tabiya kama alivyo sema katika Qur'aan (kwa mujibu wa tafsiri):

Sema! (Ewe Muhammad) Najilinda kwa Bwana wa watu, Mola wa watu, Mfalme wa watu.

Na katika hadeeth ya Mtume (Sallallaahu 'alayhi wasallam), aliposema:"Ewe Mola, Ipe nafsi yangu uchaji Mungu na Uitakase, kwani Wewe ndiye Mbora wa Mwenye kuitakasa nafsi, Wewe ndiye kipenzi chake na ndiye mwenye kuimilkia".

Ndio sababu yakanasibishwa malezi kwa Allaah ikasemwa malezi ya ki-Mungu